JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU MKOA
Mtaa wa Uzunguni,
S.L.P 37,
37101 SHINYANGA,
Tanzania.
Simu: (028) 2762630
Nukushi: (028) 2763358

APRILI 22, 2020.

TAARIFA KWA UMMA.

TAKUKURU SHINYANGA YAOKOA SH. 118,851,957/= KUTOKA VYAMA VYA USHIRIKA NA SACCOS.

Hii ni taarifa ya kazi zilizofanywa na TAKUKURU mkoa wa Shinyanga katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 (Januari-Machi 2020).

Pamoja na kazi nyingine za kawaida za TAKUKURU ikiwemo Uchunguzi, Elimu kwa umma, Kuzuia Rushwa, Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuendesha kesi zilizofunguliwa mahakamani kwa makosa mbalimbali ya Rushwa, TAKUKURU mkoa wa SHINYANGA iliendelea kufuatilia kwa kina madeni ya wakulima wa pamba, madeni ya Chama cha Ushirika cha Kahama (**KACU**) na Saccos ya Walimu Kahama.

Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2020 TAKUKURU mkoa wa Shinyanga iliendelea kukusanya madeni kwa AMCOS zilizokuwa zinadaiwa baada ya viongozi wa kufanya ubadhilifu ambapo AMCOS kumi (10) zilikuwa bado zina madeni ambazo ni **LAGANA, MUHUNZE BULUBA, BUZINZA, LAHAYABALIMI, NG'WASHINONG'HELA, NYENZE** na **KALITU** za wilayani Kishapu, **LYABUSALU, MWASINGU** na **IBADAKULI** za wilaya ya Shinyanga zilizokuwa zinadaiwa fedha na wakulima wa pamba kiasi cha **Sh. 73,938,080/=.**

Hivyo basi, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa Shinyanga wa kwa robo ya tatu ya mwaka 2019/2020 iliweza kukusanya madeni ya fedha za AMCOS kwa viongozi wa AMCOS waliofanya ubadhilifu wa fedha za wakulima katika wilaya ya Kishapu na Shinyanga fedha za msimu wa mwaka 2018/2019 na kufanikiwa

kurejesha kiasi cha **Sh. 11,523,200/=** kutoka kwa viongozi hao wa AMCOS fedha ambazo zitagawiwa kwa wakulima wa pamba hivi karibuni.

Aidha viongozi wa AMCOS ya Ibadakuli ambao wamekaidi maelekezo ya kurejesha fedha walizozifuja kiasi cha **Sh. 24,834,000/=** wamefikishwa mahakamani na kesi ya jinai dhidi yao inaendelea katika mahakama ya Wilaya ya Shinyanga.

Vilevile katika kipindi cha robo ya tatu ya Januari hadi Machi, 2020 TAKUKURU mkoa wa SHINYANGA ilifanya ufuatiliaji wa madeni uliohusisha Uchunguzi wa Chama cha ushirika KAHAMA CO-OPERATIVE UNION (KACU) na SACCOS ya Walimu KAHAMA.

Fedha ambazo zinafanyiwa uchunguzi ni jumla ya **Sh. 452,395,198/=** ambapo kiasi cha **Sh. 108,107,816/=** ni chama cha SACCOS ya Walimu KAHAMA, na kiasi cha **Sh. 344,287,382/=** Chama cha ushirika KAHAMA CO-OPERATIVE UNION (KACU) ambapo Uchunguzi ulibaini kuwa vyanzo vya madeni katika chama cha Ushirika cha KACU ni Mikopo ya watu binafsi ambayo chama kiliwakopesha,

Ushuru wa mazao ambao unalipwa na kampuni za ununuzi wa mazao, Mikopo ambayo chama kilikopesha vyama vya msingi vya wakulima (AMCOS) mbegu na pembejeo, mikopo ambayo chama kiliwakopesha wanunuzi wa mazao, na vyama vya ushirika vya Mikoa mbali mbali kwenye ufunguzi wa masoko kitaifa shughuli zilizofanyika KAHAMA mwaka 2018.

Pia uchunguzi ulibaini kuwa vyanzo vya madeni katika SACCOS YA WALIMU ni mikopo isiyo rasmi ambayo imechukuliwa na viongozi na baadhi ya wanachama, wanachama waliokoma uanachama kwa kustaafu au kuacha kazi kuondoka na madeni ya chama.

Hivyo Jumla ya kiasi cha **Sh. 107,328,757/=** kimeokolewa hadi kufikia tarehe 17. 04.2020, ambapo kiasi cha **Tsh. 4,776,300/-** kutoka SACCOS ya walimu KAHAMA, na jumla ya **Sh. 102,552,457/=** zimeokolewa toka chama cha ushirika KACU. Kati ya fedha za KACU Tsh **102,552,457/=** zilizookolewa kiasi cha **Sh. 75, 228,157/=** ziko kwenye akaunti ya KACU na Tsh. **27,324,300/=** ziko TAKUKURU (W) KAHAMA. Kati ya fedha **Sh. 4,776,300/-** za SACCOS ya walimu Kahama, **Sh. 910,000/-** ziko kwenye akaunti ya SACCOS na **Sh. 3,866,300/=** ziko TAKUKURU (W) KAHAMA.

Hivyo kwa ujumla TAKUKURU mkoa wa SHINYANGA imeokoa jumla ya **Sh. 149,355,607/=** fedha za AMCOS na SACCOS ya walimu Kahama kuanzia mwezi Oktoba, 2019 hadi 17, Aprili, 2020 ambapo kiasi cha Sh. **30,503,650/=** kati ya hizo **Sh. 149,355,607/=** ziliokolewa katika robo ya pili ya Oktoba-Desemba ya mwaka 2019/2020 na **Sh. 118,851,957/=** zimeokolewa katika kipindi hiki cha Januari-Machi, 2020. Hivyo Uchunguzi unaendelea kufuatilia madeni ya fedha zilizobaki ambazo kiasi cha **Sh. 62,414,880/=** madeni ya AMCOS za Wilaya ya Shinyanga na Kishapu, na kiasi cha **Sh. 241,734,925/=** madeni ya chama cha ushirika **(KACU)** na kiasi cha **Sh. 103,331,516** madeni ya SACCOS ya walimu Kahama

Kwa upande wa Dawati la Kuzuia Rushwa, TAKUKURU mkoa wa Shinyanga imeendelea kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayopewa fedha za Serikali na ufadhili wa wadau wa maendeleo. TAKUKURU Shinyanga ilifuatilia matumizi ya fedha za miradi **saba ya Elimu** yenye thamani ya jumla ya **Sh. 324,238,647/=** ambapo uchambuzi wa kina katika matumizi ya fedha hizi unaendelea na pale itakapobainika kuna ubadhilifu sheria itachukua mkondo wake.

Sambamba na hilo kwa kipindi husika ofisi imefanya kazi tano (05) za uchambuzi wa mfumo kwenye mifumo miwili ambayo ni mfumo katika usimamizi na uendeshaji wa AMCOS na mfumo wa usimamizi na udhibiti na uhifadhi za wanyama pori(wild protected area) na kutoa ushauri wa namna ya kuziba mianya ya Rushwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11 ya Mwaka 2007 kifungu cha 7.

Kwa upande Dawati la uchunguzi, TAKUKURU mkoa wa Shinyanga kwa kipindi cha robo ya tatu Januari–Machi cha mwaka wa fedha 2019/2020 tumepokea taarifa 76 ambazo baadhi uchunguzi umekamilika na nyingine bado unaendelea.

Kwa mujibu wa taarifa tulizopokea idara zilizolalamikiwa ni kama ifuatavyo: Ushirikika (24), Serikali za Mitaa (15), Madini (8), Polisi (7), Ardhi (6), Mahakama (5), Elimu (4), Afya (3), Sekta binafsi (2) na Siasa (1).

Kesi zinazoendelea mahakamani ni 24 kati ya hizo kesi mpya ni (5) na hakuna kesi iliyoamuliwa. Mchanganuo wa kesi zinazoendelea mahakamani kisekta ni kama ifuatavyo; serikali za mitaa kesi (12), Elimu kesi (4), Idara ya Afya kesi (3),

Uhamiaji kesi (1), NIDA (1), Michezo (1) na Taasisi za fedha (1) na Mahakama (1).

Kwa upande wa Dawati la Elimu kwa Umma, Taasisi imeendelea na jukumu lake la kuelimisha umma huku ikitoa kipaumbele kuelimisha wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kufanya kazi zifuatazo;

NA	KAZI ZILIZOFANYIKA	IDADI
1.	Semina.	11
2.	Mikutano ya hadhara.	16
3.	Ufunguzi wa klabu za wapinga rushwa kwa shule za msingi, sekondari na vyuo.	07
4.	Uimarishaji wa klabu.	42
6.	Vipindi vya redio.	01
7.	Habari/Makala.	06
8.	Maonesho.	03
10.	Mikutano na vyombo vya habari.	01
Jumla ya wananchi 20,212 walielimishwa.		

MIKAKATI YA UTENDAJI KAZI WA TAASISI KWA KIPINDI CHA MWEZI
APRILI HADI JUNI, 2020.

- Kufuatilia madeni ya fedha kwa AMCOS zote zinazodaiwa katika mkoa wa Shinyanga na SACCOS ya walimu Kahama.

- Kufanya chunguzi za vitendo vya rushwa na kuwafikisha mahakamani wahusika.

WITO

Kwa kupitia mkutano huu naomba nitoe wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Shinyanga kuwataka waendelee kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kama ambavyo wamekuwa wakifanya ili kuhakikisha kuwa tunaondoa kero ya rushwa katika Mkoa wetu.

Mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandishi wote wa habari mkoa wa Shinyanga kwa kushiriki kwenu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Imetolewa na Hussein M. Mussa Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.

Jedwali "A" FEDHA ZA WAKULIMA WA PAMBA MSIMU 2018/19 ZILIZOOKOLEWA NA TAKUKURU-SHINYANGA KWA ROBO YA TATU YA MWAKA 2019/2020.

S/No	JINA LA AMCOS	FEDHA ILIYOFUJWA	WAKULIMA WANAODAI	FEDHA ILIYOOKOLEWA	DENI BAKI LA WAKULIMA
1	Ng'washinong'hela	Tsh. 1,706,000/-	01	Tsh. 1,542,000/-	Tsh. 164,000/-
2	Nyenze AMCOS	Tsh. 1,003,150/-	01	Tsh. 302,200/-	Tsh. 700,950/-
3	Lagana AMCOS	Tsh. 17,460,080/-	8	Tsh. 2,180,000/-	Tsh. 15,280,080/-
4	Kalitu AMCOS	Tsh. 24,588,800/-	41	Tsh. 400,000/-	Tsh. 24,188,800/-
5	Muhunze Buluba	Tsh. 3,039,050/-	12	Tsh. 200,000/-	Tsh. 2,839,050/-
6	Buzinza AMCOS	Tsh. 6,692,000/-	24	Tsh. 1,745,000/-	Tsh.4,947,000/-
7	Lahayabalimi	Tsh. 9,400,000/-		Tsh. 1,754,000/'	Tsh. 7,655,000/-
8	Mwasingu AMCOS	Tsh. 10,040,000/-	12	Tsh. 3,400,000/-	Tsh. 6,640,000/-
	JUMLA KUU	**Sh. 73,938,080/-**	**99**	**Sh. 11,523,200/-**	**Sh. 62,414,880/-**

Jedwali "B" FEDHA ZA SACCOS YA WALIMU KAHAMA ZILIZOOKOLEWA NA TAKUKURU-SHINYANGA KWA ROBO YA TATU YA 2019/2020.

NA.	WILAYA	JINA LA CHAMA KIKUU, MSINGI, SACCOS	MUDA WA KUANZA UCHUNGUZI	MDAIWA	KIASI [TSHS.]	KIASI KILICHOOKOLEWA [TSHS.]	SALIO [TSHS.]
01	kahama	chama cha walimu saccos	mwezi januari, 2020	Viongozi na baadhi ya wanachama	18,393,675	3,866,300	14,527,375
				Waliokuwa Wanachama wa SACCOS	68,622,638	910,000	67,712,638
				Halmashauri (w) Msalala	6,413,610	-	6,413,610
				Halmashauri (w) Ushetu	5,975,918	-	5,975,918
				Halmashauri Mji Kahama	8,701,975	-	8,701,975
				JUMLA	**108,107,816**	**4,776,300**	**103,331,516**

Jedwali "C" MADENI YA KAHAMA CO-OPERATIVE UNION (KACU) FEDHA ZILIZOOKOLEWA NA TAKUKURU-SHINYANGA KWA ROBO YA TATU YA MWAKA 2019/2020

Na.	MDAIWA	MAELEZO	KIASI ANACHODAIWA	KIASI ALICHOLIPA	KIASI KILICHOBAKI
1.	Alliance one tobacco Ltd	Ushuru wa tumbaku	68,688,157	68,688,157	NIL
2.	Magefa grower Ltd	Ushuru wa tumbaku	9,441,965	NIL	9,441,965
3.	Kahama oil mills	Ushuru wa tumbaku	6,524,300	6,524,300	
4.	Tanzania leaf tobacco co Ltd (TLTC LTD)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	4,732,800	NIL	4,732,800
5.	Premium tobacco activate (PATL LTD)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	4,732,800	NIL	4,732,800
6.	Japanase tobaco international leaf service (JTILS LTD)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	4,732,800	NIL	4,732,800
7.	Western zone Tobacco Cooperative union (WETCU)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	1,020,000/=	NIL	1,020,000/=
8.	Lake Tanganyika Cooperative union (LATCU)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	1,020,000/=	1,020,000/=	NIL
9.	Chunya Tobacco Cooperative union (CHUTCU)	Mchango wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku	1,020,000/=	1,02000/=	NIL
10	Tobacco	Mchango	3,500,000/=	3,500,000/=	NIL

.	cooperative joint enterprise (TCJE LTD)	wa ufunguzi wa masoko ya Tumbaku			
11.	Fresho group of companies		15,861,120/=	NIL	15,861,120/=
12.	Safari Manjala	Mkopo binafsi	14,000,000/=	12,000,000/=	2,000,000/=
13.	Richard Paulo	Mkopo binafsi	1,000,000/=	NIL	1,000,000/=
14.	John Mwandu	Mkopo binafsi	350,000/=	NIL	350,000/=
15.	Mussa Ally	Mkopo binafsi	350,000/=	NIL	350,000/=
16.	Bodi ya Tumbaku - Kahama	Mkopo	6,000,000/=	6,000,000/=	NIL
17.	Warles Mhindi	Mkopo binafsi	1,000,000/=	1,000,000/=	NIL
18.	Paulo Mayala	Mkopo binafsi	500,000/=	500,000/=	NIL
19.	Yilagela Chabili	Mkopo binafsi	2,270,000/=	1,300,000/=	970,000/=
20.	Vyama vya msingi vya Pamba	Pembejeo	56,725,060/=	NIL	56,725,060/=
21.	Vyama vya msingi mbegu alizeti	Pembejeo	32,168,084/=	NIL	32,168,084/=
22.	Uyole Amcos	Pembejeo	6,000,000/=	NIL	6,000,000/=
23.	Nyenyela Amcos	Pembejeo	35,505,096/=	NIL	35,505,096/=
24.	Kasandalala Amcos	Pembejeo	66,145,200/=	NIL	66,145,200/=
25.	Tembo Amcos	Pembejeo	1,000,000/=	1,000,000/=	NIL
		JUMLA	**SH. 344,287,382**	**SH. 102,552,457/=**	**241,734,925/=**